

*Utenzi huu uliandikwa na Bi Haiba Rajabu Tambwe, wa Tabora, Tanzania akizungumzia mapenzi ya undugu katika maisha ya kila siku, hususan majonzi ya babayake mkubwa Mzee Omari Tambwe, kwa kuondokewa na mdogo wake Rajabu Salehe Tambwe, ambaye pia alikuwa mshairi na alifariki tarehe 26, Februari 1996 .*

## MADHILA

1. Madhila yasikufike, na upweke uwe kwako.  
Kesho kwako ni mwaka kesho, jibu kichwani haliko.  
Wawili huwa ni wale, japo kiziwi kwa kipofu.  
Kutwa moja ipitapo, huweza amua jambo.  
Lisitengemae hapo, bali haliharibiki papo.
2. Rajabu alikuwapo, Omari kwake kicheko.  
Yaleo siyo ya juzi, upweke Omari uko.  
Kichwani akili ipo, usoni mwake mzunguuko.  
Vitoto na vitukuu, kwake ni mkusanyiko.  
Vipi ushauri wake, madhila kwake mazito.
3. Tabora ni sokomoko, baraza halikutimu.  
Urambo hakukaliki, simu zao wakahitimu.  
Leo Dar si juzi, kusali wakihimizana.  
Madhila yasikukute, na upweke uwe kwako.
4. Wawili wenyeji hawa, katu hawakutengana.  
Wageni wao ni sisi, kilanja wetu ni Boi.  
Mgeni kwako mgeni, si sawa na nduguyo.  
Japo akuenzi sana, Jamani ni zito tengano hilo.  
Mengine tumsamehe, na dua kumuomba.
5. Siyeye wala siwewe, asemeza na moyowe.  
Hakika wewe si Kisamba, kama yapo siyo yule.  
Yule alimzowea kwa makuzi na tabia.  
Zizi lao hao moja, kwa Salehe walizaliwa.  
Vipi leo hii kioja, bura yake si rehani.  
Wageni kwake wengine, kamwe hatawazowea.
6. Walijishika mikono, wote waliambatana.  
Mengi kwake simakusudi, bali sononeko nawaambia.  
Hakika wawili wale, japo vitoto vichanga.  
Huyu akilialia, Mwenziye humsikilizia.  
Leo hii nani kwake, yu bora kuliko yule?
7. Wakiitwa Wamanyema, kwa baba na mama yao.  
Asili yao ni Kongo, simulizi wakitwambia.  
Lilobaki kundi, nasaba aruba mia.  
Umekithiri uchuro, aibu hata simuliya.  
Wengine warefu sana, wengine vifupi mno
8. Omari akiangalia, kuwafahamu ni ngondo.  
Alimjua kwa mwendo, pamwe na sauti chondo.  
Uwe usiku mzito, shindoze kwake ni tundo.  
Leo hii shauri zito, huo kwake ni uvundo.  
Wengine waziwa nyasa, walobaki wa kigoma.
9. Huku wako mbelele, na kule wanamigebuka.  
Hawafanani waw ili milele, na japo wote ni samaki.  
Ladhani huwa tofautile, na majini ni maskani.  
Hawa wanamiba tele, kumla umashakani.  
Wale ni watanganyika, na hawa wa Nyasalandi.
10. Tamani hapa kikomo, maneno yameniishia.  
La-haula, kufa kiume, si rahisi simuliya.  
Yakikupitiya mbali ni kwake, na wala si la kaya.  
Leo amkumbukia kwake, Salehe, na Yusufu Kaka.  
Akija jii namia Omari ajililia, nyuma amebakia.

*Haiba Rajab Tambwe  
Tabora-Tanzania  
Julai 2002*